7. Pigo
la kwanza litamwagwa juu ya watu gani, namna ya hili pigo ni nini? Ufunuo16: 2.

8. Je, namna ya pigo la pili, la tatu, la nne na la tano? Ufunuo 16:3, 4, 8, 9, 10.

9. Madhara ya mwisho ya pigo la sita na la saba ni nini? Ufunuo 16:12-21.

*******************************

**Somo La Desemba 7, 2024 (Kislev 6, 5785)**

## JE! NI WENGI WATAOKOLEWA?

**Somo Kuu: Luka 13: 23-30.**
**Fungu La Kukariri: Luka 13: 23-24.**

1. Ni swali gani ambalo mwanafunzi alimwuliza Yahshua wakati mmoja? Luka 13:23.
2. Jibu lake lilikuwa ni lipi? Luka 13:24; Mathayo. 7:13, 14.
3. Yahshua alisemaje kuhusu siku za Nuhu kuhusiana na kuja kwake? Mathayo. 24:37.
4. Hali ilikuwa nini katika siku za Nuhu na Elohim alihisije kuhusu hiyo hali? Mwanzo 6: 5, 7.
5. Je, ni wengi waliokolewa? Mwanzo 7: 7.



7. Nani ambaye tunapaswa kutii katika Kanisa? Waebrania 13:17; 1 Wathesalonike 5:12, 13.
8. Ni heshima kiasi gani wao wanastahili, na tunafaa kuaamini mashtaka yote? 1 Timotheo 5:17-19.
9. Nani ambao tunapaswa kutii nje ya Kanisa? Tito 3:1.
10. Mtazamo wetu kwa wanaotawala ni upi? 1 Timotheo 2:1-3;1 Petro 2:12-19.
11. Ni taarifa ipi maalumu Samweli alijulisha mfalme Sauli kuhusu kutii? 1 Samweli15:22.
12. Kwa nini Sauli alikataliwa na Elohim kama mfalme? Aya ya 23.
13. Je, neno la Bwana linatufundisha kwamba wasiotii wataadhibiwa hata katika maisha haya? Jinsi gani thawabu yetu itaamuliwa? Warumi 2:6-11.
14. Tumeshauriwa kufanya nini katika Waebrania 2:1-3?

*******************************



8. Bwana atakuja mahali gani atakaporudi duniani? Zek. 14:4
9. Ni nani atakayekuwa Mfalme wa ulimwengu wote wakati huu na baadaye? Zek. 14:9; Ufu. 11:15.
10. Je! Ni nini kilichosemwa zaidi kuhusu Makao Makuu ya Ufalme Wake? Je, kutakuwa na ongezeko la amani wakati huu? Zaburi 110:1-6; Isaya 9:6, 7.
11. Bwana na Mwokozi Yahshua Masihi atatawala akiwa Mfalme kwa muda gani? Ufu.20:4.

*******************************



***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao" Zaburi 122:6***



# Masomo Ya Bibilia

***kwa***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th day)**

Robo Ya Nne
2024

Ya
Julai, Agosti, Septemba.
**(Tishrei, Cheshvan, Kislev)**

Watenda kazi wanahitajika,
Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

## Somo La 26 Oktoba, 2024 (Tishrei 24, 5785)
# MAISHA YAKO NI NINI?

**Somo Kuu: Zaburi 39.**
**Fungu La Kukariri: Yakobo 4:14**

1. Je! Daudi aliwahi kueleza ukweli gani wa milele? 1 Sam. 20:3.
2. Je, Ayubu alielezea ukweli huu kwa njia gani? Ayubu 3:8
3. Yakobo alisema nini kuhusu ufupi wa maisha? Yakobo 4:14, 15.
4. Yahshua alitoa ombi gani kwa watu wa nyakati zake? Yohana 6:27, 50, 51
5. Tunapaswa kuweka hazina yetu wapi? Mat. 6:19, 20.
6. Ni ujumbe gani ambao bado unafaa kwa leo? Efe. 5:14-17.
7. Kwa kuwa maisha yetu ni mafupi na hayana uhakika, tunapaswa kuwa tunafanya nini? Yohana 4:35, 36.
8. Tunapaswa kufikiria nini sikuzote? Yohana 9:4
9. Tunaonywaje kuhusu kuishi maisha ya ubinafsi? 1 WaKor. 10:24; Wafilipi. 2:4



## Somo La Novemba 30, 2024 (Cheshvan 29, 5785)
# TAHADHARI KABLA YA UHARIBIFU

**Somo Kuu: Ezekieli 33: 1-29.**
**Fungu La Kukariri: Ezekieli 33: 6.**

1. Je, Bwana alisema nini kuhusu tahadhari kwa wale wasiotii kuwa ghadhabu yake haitakuja kwa watu wake? 2 Mambo ya nyakati 19:9, 10.
2. Kama watumishi wa Elohim hawatawaonya waovu, na waovu kupotea katika uovu wao, madhara kwao yatakuwa yapi? Ezekieli 33: 6.
3. Wakati tahadhari imetolewa, lakini ikakosa kufuatwa, na waovu wakaendelea katika uovu na kuangamia, ni nini itakuwa matokeo? Ezekieli 33:9.
4. Ni nini itakuwa matokeo ya kutotii ujumbe na kukosa kutoka Babeli? Ufunuo 18:4 sehemu ya mwisho. Linganisha pia Ufunuo 14:10 sehemu ya kwanza.
5. Ujumbe wa malaika wa tatu ni tahadhari maalum dhidi ya kupokea alama ya mnyama. Nini itakuwa madhara ya kukataa huu ujumbe? Ufunuo 14:10.
6. Ni malaika wangapi watayamwaga mapigo, na ni juu ya eneo kiasi gani watafikia? Ufunuo 16:1.



## Somo La Oktoba 5, 2024 (Tishrei 3, 5785)
# NI LAZIMA MTU AZALIWE TENA

**Somo Kuu: Waefeso 3**
**Fungu La Kukariri: Yohana 3:3**

1. Ni nini nabii Malaki alisema kuhusu mjumbe ambaye atatangaza Bwana? Bwana Yahshua angefanya nini wakati angelikuja? Malaki 3:1-3.
2. Ni nini Isaya alitabiri kuhusu huyu mmoja aliyechaguliwa kuandaa njia kwa ajili ya Mkombozi wa dunia aliyengojewa kwa muda mrefu? Isaya 40: 3.
3. Wakati Mjumbe huyu ambaye manabii walizungumza kumhusu angelikuja, uzito wa ujumbe wake ungekuwa upi? Mathayo 3:1-3.

   **Maelezo**: Watu waliokuja kwa Yohana Mbatizaji wakitamani kubatizwa, si kwamba walikubali ukweli tu, lakini pia walikuwa na huzuni kwa sababu ya dhambi zao na walitubu na kuikiri kwa Elohim. Wale waliokataa kutubu dhambi zao za zamani walikuwa wanarudishwa.
4. Yohana Mbatizaji alisema nini kuhusu Yahshua, ambaye alikuwa akitayarisha njia yake? Mathayo 3:10-12.
5. Muda mfupi baada ya Yahshua kuanza huduma yake, ni nani ambaye alikuja kwake? Alisema nini? Yohana 3:1, 2.



## Somo La Desemba 28, 2024 (Kislev 27, 5785)
# MFALME AJAYE, UFALME WAKE

**Somo Kuu: Ufunuo 20:1-6; Isaya 11:1-9**
**Fungu La Kukariri: Luka 12:32**

1. Je! mbingu zitamzuia Bwana na Mwokozi wetu Yahshua Masihi hadi lini? Matendo 3:20, 21.

   **Maelezo**. "Nyakati za Kurejeshwa" haimaanishi wakati wa Kuangamizwa kwa kila kitu kilicho hai, bali ni urejesho wa ulimwengu mzima kurudi kwenye Paradiso ya Edeni; ilivyokuwa kabla mwanadamu hajatenda dhambi. Mwanzo 8:21.

2. Atakaporudi Bwana wetu atakuja na nini pamoja naye? Ufu. 22:12; Isaya 62:11.
3. Ufalme huo wa utakatifu utaendelea hadi lini? Danieli. 7:13, 14
4. Ufalme huo utakuwa wapi na utapewa nani? Danieli 7:27
5. Huyu "Binti Sayuni" analinganishwa na nini? Yeremia 6:2; Ufu. 19:7, 8
6. Mwanamke huyu, mfano wa kanisa la kweli, anaelezewa wapi kwa uhakika zaidi? Ufu. 12:1
7. Je! Ni nini kilichosemwa kuhusu imani ya kanisa hili la Mabaki? Ufu. 12:17.

na kwa sababu Farao hakuwaruhusu watu waende.

9. Je! Yohana aliwaona wapi wale waliopata ushindi juu ya yule mnyama na juu ya jina lake? Ufu. 15: 2, 3

**Maelezo**: Kuna maoni mengi tofauti juu ya mahali bahari hii ya glasi iko, ni mahali pa kukimbilia, ambapo mapigo hayataanguka.

10. Wakati malaika alimwaga bakuli lake juu ya mito na chemchemi za maji, malaika wa maji alisema nini? Ufu 16: 5-7
11. Janga la mwisho litakapoanguka, kundi moja la watu wa dunia litafanya nini? Ufu 16:21.
12. Je! Jinsi gani matukio ambayo yalitokea kwa wana wa Israeli yanahusishwa na matukio ambayo yatatokea mwisho wa wakati huu? 13. 1 Kor. 10: 5,11
13. Kabla ya Waisraeli kuondoka Misri, walipata fadhili machoni pa Wamisri na ni kwa kusudi gani? Kutoka 12: 36

*******************************



10. Ni nini imesemwa kuhusu Mwokozi wetu mpendwa? 2 WaKor. 8:9; Rum. 15:3.

11. Ni mfano wa nani hatupaswi kufuata? Luka 12:18, 21 .

12. Kila mfuasi wa Masihi Yahshua anapaswa kuhisije? 2 WaKor. 5:20

13. Ni ahadi gani huambatana na kila mfanyakazi? Zab. 126:5, 6.

14. Tuzo letu la mwisho litakuwa gani? Dan. 12:3.

********************************

**Somo La Novemba 2, 2024 (Cheshvan 1, 5785)**

## MAISHA YA MILELE

**Somo Kuu: Yohana 3: 1-21.**
**Fungu La Kukariri: Yohana 10:10.**

1. Je! Masihi alikuja kuhukumu ulimwengu? Yohana 3:17.

2. Je! Ni nini kinachotuhukumu? Yohana 3:18.

3. Kwa nini watu wanapenda giza? Yohana 3:19.

4. Kwa nini waovu wanaogopa nuru? Yohana 3: 20, 21.

5. Ikiwa tutaamini, sisi ni nani? 1 Yohana 5: 9, 10.



watabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua, na kuishi na kutawala pamoja na Masihi kwa miaka elfu. Wakati huu Yahshua atakuwa akitawala katika kiti cha enzi cha Daudi.

5. Ni wapi ambapo wafu waovu watakuwa wakati wa utawala wa miaka elfu wa Bwana Yahshua? Ufunuo 20: 5, 6.
6. Waovu watafufuliwa? Yohana 5:28, 29.
7. Ni kwa madhumuni gani waovu watafufuliwa? 2 Petro 2:9.
8. Wakati waovu watafufuliwa ni wapi ambapo wataonekana? Ufunuo 20:11-13.

**Maelezo**. Hukumu ni kwa ajili ya waovu, wenye haki walienda katika hukumu wakati walikiri dhambi zao, kuzaliwa tena na wakawa watiifu kwa neno la Bwana; hivyo wao walipita kutoka mautini kuingia uzimani na wakawa washiriki wa familia ya Elohim. 1Tim 5:24, Yohana 5:24.

9. Je, hatima ya waovu itakuwa ipi? Ufunuo 20:13-15, 21:8

******************************



**Maelezo**: Inawezekana kwamba Nikodemo aliona aibu kuonekana na Yahshua, na kwa hivyo alichagua kuja usiku, wakati hatari ya kuonekana na marafiki zake wasioamini ingekuwa dogo? Hii inalingana na watu katika siku hii na wakati huu ambao wamesikia kuhusu Bwana, lakini wanaogopa kukiri kwake, katika uwepo wa marafiki zao wa kidunia.

6. Jinsi gani Yahshua alijibu Nikodemo? Yohana 3:3.
7. Wakati Nikodemo hakuelewa kuhusu kuzaliwa upya na kusema “Jinsi gani mambo haya yanawezekana?” Yahshua alimjibu vipi? Yohana 3:10-12.
8. Jinsi gani Yahshua alionyesha kwamba kuna umuhimu kwa mtu kuzaliwa upya? Yohana 3:5-8.
9. Ni nini ingine maandiko matakatifu ya Elohim yanasema kuhusu kuzaliwa upya? Yohana 1:12, 13; 1 Petro 1:23.
10. Ni kwa sababu gani mwana wa Elohim alidhihirishwa? 1 Yohana 3:5-9.

**Maelezo**: Utakaso (Masihi ndani yetu) na kubakia katika kweli kutokana na mateso na majaribio, ni njia yetu ya pekee yenye usalama, uhakika na nguvu.

6. Je! Tutapata ushahidi gani? 1 Yohana 5: 9, 10.
7. Je! Sisi waumini tunapataje uzima wa milele? 1 Yohana 5:11.
8. Je! Tunapata uzima wa milele kupitia nani? 1 Yohana 5:12.
9. Je! Uzima wa milele umetiwa muhuri na nani? Waefeso 1:13.
10. Je! Ni nini hatupaswi kufanyia Roho? Waefeso 4:30.
11. Ni lini tutaweza kudai kuwa wana wa Bwana? 1 Yohana 3: 1, 2.
12. Je! Sisi WaMasihi tunangojea nini? Warumi 8:19.

**Maelezo**. - Imani ndio kiini cha mambo yanayotarajiwa. Ni imani hutuongoza kwa Bwana. Wengine wanangojea hisia; tunapompokea Yahshua, tunajua kuwa sisi ni wenye dhambi na kwamba Yahshua ni Mwokozi wetu. Tunazungumza naye katika maombi juu ya hali yetu ya kupotea, tunakiri na kutubu, na Yeye hutupea ushuhuda katika mioyo yetu kwamba tumesamehewa, na kwamba Yeye huchukua makao yake katika maisha yetu na hufanya vitu vyote kuwa vipya, Msifuni!

********************************



Sodoma na Gomora, kabla ya kuangamizwa; Aliwaonya Tiro na Sidoni; Alionya Ninawi na Babeli.

3. Je! Sauti kutoka nje ya hekalu mbinguni ilisema nini kwa malaika saba, na mapigo yanaanguka juu ya nani? Ufu 16: 1,2.
4. Je! Asili ya kila aina ya janga ni nini? Ufu.16: 3-14.

**Maelezo**: Mahali paitwapo "Amagedoni" iko katika bonde la Yezreeli, kama maili hamsini kaskazini magharibi mwa Yerusalemu.

5. Ni nani anayeshinda kwenye vita hivi na ni kwa jinsi gani? Ufu 16: 17-21
6. Je! Hali ya jumla ya watu wa dunia nzima wakati hukumu hizi zinaanza itakuwa gani? Isa. 42: 4,5; 26: 21; Mat. 24: 37-39

**Maelezo**: Tunaambiwa kwamba katika siku za Nuhu, uovu ulikuwa mwingi juu ya ulimwengu na kwamba "kila fikira za mawazo ya mioyo ya watu ilikuwa mbaya tu kila wakati" Mwa 6: 5.

7. Je! Watu wenye haki watateseka na mapigo haya, Zaburi 91: 3-11
8. Je! Mapigo yaliyoanguka juu ya Wamisri yaliwaangukia Waisraeli? Kutoka 8:22; 9: 6, 26; 10: 23; 11: 7.

**Maelezo** . Sababu ya mapigo haya juu ya Wamisri ilikuwa ni jinsi walivyowatendea Israeli,



11. Katika unabii wa Danieli wa mwisho wa wakati huu, ni makundi gani mawili ya watu yametajwa? Danieli 12:10.

********************************

**Somo La Oktoba 12, 2024 (Tishrei 10, 5785)**

## MAHUBIRI JUU YA MLIMA

**Somo Kuu: Mathayo, sura ya 7**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 7:21.**

1. Mwokozi alilaani mazoea gani mabaya? Mathayo 7:1-3.
2. Ni nini kwanza inafaa kufanyika kabla ya kujaribu kurekebisha wengine? Mathayo 7:4, 5; Mathayo 5:23, 24.

**Maelezo:** Ni ukosefu wa Roho ya kweli ya uvumilivu na upendo ambayo uongoza mtu kusisitiza makosa kwa wengine, na hufanya mlima kutoka kwa mlima wa fuko. Kulaumu na kuabisha kamwe hakujawahi kuokoa nafsi iliopotoka, lakini wengi hupotoka zaidi kwa hayo. Roho nzuri ya kukaripia kwa upole, kukaripia aliyekosea na kwa faragha kwa kuonyesha upendo wa huruma, ndiyo itaweza kumrejesha mtu katika njia nyembamba.



8. Je, wafu wanaweza kumsifu Bwana? Zaburi 115:17.
9. Je, kuna ukumbusho katika mauti na kaburini? Zaburi 6:5.
10. Je! Ni nini kilichosemwa tena juu ya wale waliokufa katika Bwana? Ufunuo 20:6.

********************************

**Somo La Desemba 21, 2024 (Kislev 20, 5785)**

## UFUFUO

**Somo Kuu: 1 Wakor. 15: 1-58.**
**Fungu La Kukariri: 1 Wakor. 15:22**

1. Kila mtu atafufuliwa? Yohana 5:28, 29.
2. Ni lini watakatifu watafufuliwa wakati kwa uzima wa milele? 1 Wakorintho 15:22-23; Ufunuo 20:4-6; 1 Watheso 4:16.
3. Je, ni nini kitatokea kwa watakatifu ambao watakuwa hai katika kuonekana kwa Yahshua? 1 Watheso 4:17; 1 Wakorintho 15:51-53.
4. Ni wapi ambapo watakatifu watakaofufuka watakaa, na nini itakuwa kazi yao wakati wa milenia?Ufunuo 5:10; Danieli 7:27.

**Maelezo**. Ni baraka za ajabu gani watapata waamini wote katika Masihi Yahshua! Wote waliokufa katika Bwana watahuishwa katika kuonekana kwa Yahshua, watakatifu walio hai

9. Ili tuweze kuyafikia yaliyo juu ambayo tunayatamani, ni nini tunahitaji kujua? Wafilipi 3:10, 11.
10. Tunapaswa kusahau nini, na tunapaswa kuyafikia mambo gani yaliyo mbele? Wafilipi 3:13.
11. Kama tunapoendelea kukaza mwendo ni nini tunaagizwa kuweka mbali, na ni nini tunachoambiwa tukitamani? 1 Petro 2: 1, 2.
12. Tunapojitahidi kushinda ulimwengu huu na tamaa za kimwili, ni nini tunaagizwa kufanya kila mara? Waefeso. 6:18.

*******************************

**Somo La Novemba 23, 2024 (Cheshvan 22, 5785)**

## HUKUMU YA MBINGU INAYOSUBIRI

**Somo Kuu: Ufunuo wa 15 sura ya**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 15: 2**

1. Je! Ghadhabu hii itamwagwa na nani duniani? Ufu. 15: 1; 16: 1.
2. Kabla ya hukumu hii kumwagwa juu ya waovu, ni ujumbe gani wa ulimwengu unaotolewa? Ufu 14: 9,10

   **Maelezo**: Baba wa mbinguni huwaonya watu kila wakati kabla ya kuwaletea hukumu. Ni matumainio Yake ya upendo kwamba watu waishi kwa furaha na kwa kutii mapenzi Yake. Alionya



**Somo La Novemba 9, 2024 (Cheshvan 8, 5785)**

## UTAJIRI WA MILELE

**Somo Kuu: 1 Timotheo 6.**
**Fungu La Kukariri: 1 Timotheo 6:11.**

1. Je! Mada ya mahubiri ya Paulo kuhusiana na utajiri ni gani, katika Waefeso 3:8 na ni onyo gani linalotolewa katika 1 Timotheo 6:17-19?
2. Je! Hali halisi ya wengi walio maskini wa mali za kilimwengu na wengine matajiri ni gani? Ufunuo 2:9, 3:15-17.
3. Ili kushiriki utajiri usioelezeka, ni maagizo gani yanayotolewa zaidi katika Ufunuo 3:18?
4. Ni nani anayesimama mlangoni, tayari sikuzote kutusaidia? Ufunuo 3:20.
5. Ikiwa sisi kupitia kuwapo kwake na msaada wake tunafanikiwa kuushinda ulimwengu na vivutio vyake, Yahshua anatoa ahadi gani kuhusiana na jambo hili? Ufunuo 3:21.
6. Ingawa Yahshua mwenyewe alikuwa maskini sana hivi kwamba hakuwa na pa kulaza kichwa Chake, je, ana uwezo wa kuwapa wengine mali halisi, na je, hajafanya hivyo? 2 Wakorintho 6:10.
7. Ni onyo gani linalotolewa kuhusu kutamani na je, maisha ya mtu yanajumuisha vitu alivyo navyo? Luka 12:15.



11. Je, nini kitatokea kwa kundi la watumishi Wake ambao hawana faida katika kumaliza kazi? Mathayo. 25:30.

*******************************

**Somo La Desemba 14, 2024 (Kislev 13, 5785)**

## BAADA YA KUFA, NI NINI?

**Somo Kuu: 1 Wathesalonike 4.**
**Fungu la Kukariri: 1 Wathesalonike 4:16.**

1. Je! Biblia inasema kifo ni nini? 1 Wathesalonike 4:13, 14.

   **Maelezo**. Wakati mtu amelala anapoteza fahamu kabisa; muda unaendelea bila kupimwa, na kazi ya ufahamu wa akili inasimamishwa kwa muda.
2. Wafu wanalala wapi? Danieli 12:2.
3. Wataendelea kulala katika mavumbi ya nchi mpaka lini? Ayubu 14:10-12; 1 Wakorintho 15:42-58.
4. Je! Ayubu alisema atasubiri nini? Ayubu 14:14.
5. Je! Atasubiri mabadiliko haya akiwa wapi? Ayubu 17:13.
6. Je! Mfalme Hezekia aliandika nini kuhusu kifo na kaburi? Isaya 38:18, 19; Zaburi 30:9.
7. Ni nini imelezewa kuhusu mawazo ya wale waliokufa? Zaburi 146:4; Mhubiri 9:5, 6, 10.



3. Ni nini imesisitizwa hapa kuhusu njia mbili za maisha, ambayo ni dhahiri leo? Mathayo 7:13, 14.
4. Kutakuwa na manabii wa uongo na walimu wa uongo katika siku za mwisho? Mathayo 7:15; Mathayo 24:24.
5. Ni jinsi gani tutawatambua? Isaya 8:20; Mathayo 7:16, 17.
6. Wahubiri wa uongo hukiri imani katika Mwokozi, na wanaweza kufanya kazi nzuri katika jina lake. Mathayo 7:22.
7. Hatima yao itakuwa ipi katika siku ya hukumu? Mathayo 7:23.
8. Je, Yahshua anasema nini kuhusu wale watakao ingia katika ufalme? Mathayo 7:21.
9. Anawalinganisha na nini wale husikia na kutenda aliyoyanena? Mathayo 7:26, 27.
10. Wale husikia tu wanalinganishwa na nini? Mathayo 7:26, 27.
11. Kumwamini Mwana tu bila kutii kutatufanya tupate chochote? Yakobo 2:19, 20; Yakobo 1:21, 22.

*******************************

8. Mtu anayeweka hazina za kidunia na si tajiri kwa Elohim anasemwa kuwa aje? Luka 12:16-21.

   **Maelezo**. Masihi halaani hazina za kidunia mradi tu mtu huyo ni tajiri kwa Elohim na anagawa pamoja Naye sehemu inayohitajika, na kwa kufanya hivyo ni kuwasaidia wale walio na uhitaji.
9. Je, watu waaminifu wa Bwana wanapaswa kujiepusha na kusaidia kazi hiyo kwa ukarimu na fedha zao kwa kuogopa kwamba wanaweza kupata uhitaji na kuteseka? Luka 12:22-30.
10. Tunawezaje kuhamisha hazina za kidunia hadi kwenye hazina za mbinguni? Luka 12:31,33,34.
11. Ni nini kinasemwa kuhusu taa zetu kuwaka na sisi kuwa tayari kupokea Bwana ajapo? Luka 12;35,36.

   **Maelezo**. Yahshua alisema amewachagua maskini wa ulimwengu huu, matajiri wa imani na warithi wa ufalme, na kwa hiyo tunaona maneno yake kuwa ya kweli hadi leo. Maskini ni watu ambao kila mara hukubali ujumbe wa injili kwa haraka zaidi katika nyanja zote za kazi.

*****************************



**Somo La Novemba 16, 2024 (Cheshvan 15, 5785)**

## URITHI ULIO HAKIKISHWA

**Somo Kuu: 2 Petro sura ya 2.**
**Fungu La Kukariri: Phil. 3:14.**

1. Je! Ni hatua gani ambazo ni muhimu katika kuutafuta uzima wa milele? Waebr. 11: 6; Matendo 3:19; Wagal. 3:27.
2. Ni tuzo gani kubwa tunapaswa kutafuta kwa bidii? Wafilipi 3:14.
3. Ili kujihakikishia uteuzi wetu, ni tahadhari gani na ushauri maalum unaotolewa? 2 Petro 1:10.
4. Kwa maisha ya bidii na huduma ya faida kwa Bwana, tunakubaliwa kuingia katika ufalme gani, na ni nini hali ya uvumulivu wa uraia wake? 2 Petro 1:11.
5. Baada ya kupokelewa kama watahiniwa wa urithi huu, ni wapi tunapaswa kuweka ari yetu? Wakolosai. 3: 1, 2.
6. Tunapaswa kutafakari nini na kuifanyia kazi kwa bidii? Wafilipi 3:20.
7. Nia ya Masihi ilikuwa imejaa mawazo ya kazi ya kuhubiri injili; na kama mfanyakazi wa wito wa mbinguni alifaidika, tunapaswa kuwa na nia gani? Wafilipi 2: 5.
8. Ili nia zetu ziwe juu ya mambo yaliyomhusu Masihi zaidi, je ni muhimu kwetu kujifunza maisha na kazi zake? Wafilipi 3: 8, sehemu ya kwanza; 2 Petro 3:18.



**Somo La Oktoba 19, 2024 (Tishrei 17, 5785)**

## TUTATII NANI

**Somo Kuu: Matendo 5:12-27.**
**Fungu La kukariri: Matendo 5:29.**

1. Ni pendekezo gani iliwekwa kwa Israeli katika mlima wa Sinai? Kutoka 19:3-6.
2. Ni nini ingewafuata wana wa Israeli kama wangetii amri hizi? Kumbukumbu la Torati 11:26, 27.
3. Licha ya ahadi hizi ambazo ni nzuri sana, jinsi gani wana wa Israeli walilifikiria hilo agano? Yeremia 31:31, 32
4. Ni somo gani tunaweza kujifunza kutoka kwa mtazamo wa Shadraka, Meshaki, na Abednego wakati wa jaribio? Danieli 3:8-26.

   **Maelezo:** Hebu tuelewe kwamba hakukuwa na uhakika wa kuokolewa, lakini waliridhika kufa katika kumtii Bwana.
5. Ni nini kilichosemwa kuhusu kutii Bwana Yahshua katika Waebrania 5:7-10?
6. Ni nani mwingine tunafaa kutii licha ya Bwana, na ahadi ya Elohim kwa ajili ya utiifu huu ni nini? Mithali 23:22; Waefeso 6:1-3.



**Maelezo**. - Kwa jumla ni roho nane zilizookolewa wakati wa mafuriko. Ingawa Noa alikuwa mhubiri, wa haki kwa miaka na miaka, hakuweza kuwafanya watu kuona uharibifu unaokuja ambao utawaondoa wote isipokuwa wamgeukie Elohim. Masihi anafananisha kuja kwake kwa pili na siku za Nuhu, na kwa kuamini maneno yake kuwa kweli, hatuwezi kutarajia wengi kugeuka kutoka kwa njia zao mbaya. Hata hivyo, lazima tuendelee kuhubiri injili kama vile Nuhu alivyofanya.

6. Ni wangapi waliokolewa kutoka miji miovu ya Sodoma na Gomora? Mwanzo 19:15.
7. Je, ni nini kilichotokea kwa mke wa Loti? Je, tunashauriwa kukumba nini? Mwanzo 19:26; Luka 17:32.
8. Je, Masihi alitoa ahadi gani kwa wachache? Luka 12:32.
9. Je, Masihi alisema nini kuhusu wale ambao wataingia katika Ufalme wa Elohim? Mathayo. 7:21.
10. Je, kutakuwa na watu wengi watakaokuwa wakiomba kuingia katika Ufalme? Mathayo. 7:22.